USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE

READY GLOBAL READINESS FOR MAJOR DISEASE OUTBREAK RESPONSE

# Maandalizi na suluhu kwa magonjwa ya mlipuko katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo : Inawezekana je kutumia mbinu marafiki wa watoto katika chanjo ?

Mahitaji ya watoto ni tofauti na ya watu wazima na hivyo inahitaji mikakati mahususi ili kuhakikisha mafanikio ya kampeni za chanjo. Woga wa sindano, maambukizi na/au madhara pamoja na taarifa potofu au ukosefu wa taarifa inaweza kuwa vikwazo.

Wakati wa kutoa chanjo zinazohusisha watoto na vijana, tumia karatasi hii ya kidokezo ili kufanya kampeni ifae zaidi mahitaji yao :

**Kumbuka : Ushauri mwingi huu unaweza kutumika wakati wa uchunguzi na matunzo . Kwa mfano, wakati wa mtihani wa damu au swab ya pua ili kuangalia maambukizi.**

## Kujaza mapengo yoyote katika taarifa :

- Kuwapa wazazi/wauguzi taarifa sahihi kuhusu ugonjwa wa kuambukiza na kuhusu chanjo, ikiwemo wapi na jinsi ya kupata chanjo kwa watoto wa rika tofauti. Kuzingatia mazungumzo juu ya ushahidi wa ugonjwa huo na matokeo yake ili kupambana na uvumi na kusita kuhusu chanjo. Hii inaruhusu wazazi na wauguzi kufanya chaguo sahihi na ridhaa yao dhidi ya chanjo.
- Kuwapa wazazi/vijana habari wanayohitaji pia ili kuwawezesha kutoa kibali sahihi.
- Kutumia lugha na miundo inayoweza kufikiwa na inayofaa kwa umri, kusoma na kuandika na/au ulemavu miongoni mwa watoto na wazazi/wauguzi. Shiriki ujumbe muhimu na unaolengwa kupitia vyombo vya habari mbalimbali ikiwa ni pamoja na maandishi, sauti, na ujumbe wa video.

## Kukabiliana na hofu/uoga na huzuni kwa watoto :

- Andaa watoto. Waelezee kinachokuleta pale na/au kwa nini unahitaji kuwapa chanjo, kipimo cha damu au kuwapa dawa. Waambie nini cha kutarajia. Eleza hatua za mchakato mzima, itachukua muda gani, ikiwa itawumiza, jinsi maumivu yatakavyokuwa. Waambie kabla ya kuwagusa. *« Ni kama kuumwa na nyuki. Utahisi nimekubana haraka. »*
- Waonyeshe kwanza. Uliza mtoto mkubwa au mtu mzima atoe damu, achanjwe au anywe dawa mbele yake ili kupunguza hofu yao.
- Kadiri inavyowezekana, mruhusu mtoto achague na/au atoe masuluhisho. Kukubaliana kwa pamoja juu ya kile kinachowezekana. *« Je, unataka kupata chanjo kwa mkono huu au mwingine? » Mkono wako wa kuandika ni nini ? Nitakuchanja kwa mkono mwingine ili usiwe na maumivu unapolazimika kufanya kazi yako ya shule. »*

- Kujaribu kugeuza kuchukua dawa kuwa mchezo. Unaweza kuimba kwa ajili ya watoto au kumuomba akuimbie. Unaweza kutumia kifaa cha simu kucheza muziki anaoupenda na kumkengeusha. Hata hivyo, mwambie kwa unyoofu kitakachompata huku akiwa amekengeushwa fikra.
- Ruhusu na uwahimize watoto wachanga kuweka vitu wapendavyo « vinyago, wanyama waliojazwa, blanketi » pamoja nao kwa faraja. Kuwezesha unyonyeshaji wakati wa chanjo ya watoto wachanga ili kupunguza maumivu.
- Wape watoto vibandiko, mihuri, beji, mipira ya kucheza au karatasi za kuchorea. Watoto wakubwa/vijana wanaweza kutaka kuchukua selfie ili kushiriki kwenye mitandao ya kijamii, kuwahimizia wenzao kupata chanjo pia.

## Toa huduma zinazozingatia mahitaji ya watoto na familia zao :

- Toa saa za huduma zilizorekebishwa kwa familia na nyakati rahisi za mikutano katika maeneo yanayofikiwa na watu wenye ulemavu.
- Shirikiska watu wenye ulemavu na mashirika yao ile kuhakikisha upatikaniji kamili wa chanjo.
- Kuhakikisha utoaji wa huduma kwa haraka ili kutosubilisha watoto. Kutanguliza chanjo kwa watoto walio katika hatari, ikiwa ni pamoja na watoto wenye ulemavu, au hali ya afya ambayo inaweza kuwafanya kuwa katika hatari zaidi ya kuambukizwa na/au kupunguza uwezo wao wa kufuata hatua za afya ya umma
- Chagua vituo vya chanjo ambavyo huruhusu watoto kutembea huku wakidumisha umbali muhimu wa kimwili kulingana na hatua za kuzuia zinazotumiwa hapo hapo.
- Pamba sehemu tofauti ili watoto waambatane na wazazi/wauguzi wao.
- Toa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya watoto wanaohitaji muda au msaada zaidi.
- Kutafuta suluhu kwa vikwazo vya kifedha na vifaa vya chanjo. Pendekeza kliniki zinazohamishwa ikiwa ni lazima.
- Chukua fursa hii kuthibitisha utolewaji wa chanjo nyingine za kawaida za utotoni ambazo huenda zilikatizwa kwa sababu ya mkurupuko au hali halisi nyinginezo.

## Shukrani

*Hii karatasi ya ushauli iliwezeshwa na usaidizi mkubwa wa watu wa Marekani kupitia Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID). Yaliyomo ni wajibu wa READY na si lazima yaakisi maoni ya USAID au Serikali ya Marekani. Wakiongozwa na Save the Children, Mradi wa READY unatekelezwa kwa ushirikiano na Kituo cha Johns Hopkins cha Afya ya Kibinadamu, Kituo cha Johns Hopkins cha Mipango ya Mawasiliano, Humanitarian Leadership Academy, na UK-Med. READY inaongeza uwezo kwa mashirika yasiyo ya kiserikali duniani kote kukabiliana na milipuko mikubwa ya magonjwa ya kuambukiza. Kwa habari zaidi, tembelea tovuti yetu katika*

**http://www.ready-initiative.org**

Johns Hopkins Center for Humanitarian Health | Johns Hopkins Center for Communication Programs | Save the Children | humanitarian leadership academy | UK-MED